JUMAMOSI - USIKU

Nilipoondoka nyumbani nilikuwa nimejaa wasiwasi moyoni, hamasa na msisimko kwenye kila nchi ya mwili wangu. Nilikuwa nafikiria mambo mengi kiasi kwamba nilikuwa kujiona kana kwamba nilikuwa ni mshiriki katika kisa cha Elfu Leyla Uleyla au kama kinavyojulikana kwa kiingereza “Arabian Nights”. Nilikuwa nimeshakivuka kizingiti cha hofu na nilikuwa tayari kwa liwalo na liwe. Wakati naelekea kwenye barabara kuu ya Morogoro nilinyanyua simu yangu ya mkononi na kubonyeza kwa haraka namba ya Freddy. Haikupita hata sekunde simu ilipokelewa.

“Freddy hapa” alijibu kwa sauti yake ya upole.
“Hi baby!” nilimuita hivyo. Nilijisikia kama binti ambaye amepata kidate chake cha kwanza. Viganja vya mikono vilikuwa vinaunyevu wa jasho kidogo.
“Hi Tina, usiniambie umeahirisha please” alisema huku akiyaachia maneno hayo yaelee hewani kama tiara huku kwa pumzi ameshikilia nyuzi yake.
“Hapana dear, niko njiani” nilimuambia.
“Safi kabisa, sasa njoo tena hadi Blue Pearl halafu ntakukuta hapo” alinielekeza.
“Kwanini tena pale” nilimuuliza kwa sauti ya kulegeza kidogo maana wazo la juzi bado lilikuwa likinisumbua na kwa hakika nisingeweza kupita eneo hilo tena bila kumfikiria Mjamaika.
“Hapana bwana, we njoo utaegesha gari lako hapo ni salama zaidi halafu nitakuchukua twende kwangu” alisema. Nilimuelewa hasa kwa sababu nilikuwa nimechukua Mercedes tena. Tulikubaliana na nilipoiweka simu chini nilizungusha macho yangu kwa mbwembwe nikijiambia moyoni mbombo jilipo kama wanavyosema Wanyakyusa. *Kazi ipo.*

Jioni hiyo ya Jumamosi hakukuwa na magari mengi kama ilivyo wakati wa siku za kazi. Sehemu mbalimbali watu walikuwa wametulia katika baa zilizoko pembezoni mwa barabara ya Morogoro wakijipongeza kwa vinywaji baridi na nyama choma. Ilikuwa ni jioni iliyotulia sana na kwa namna fulani iliwakilisha nilivyojisikia moyoni.

Haikunichukua muda kufika tena Blue Pearl ambapo mara baada ya kuegesha gari nilimuona Freddy akija kutoka kama upande wa mwisho wa kuegeshea. Nilitoka ndani ya gari nikiwa nimeshikilia mkoba wangu, simu na funguo ya gari. Nilibonyeza kitufye cha usalama kilicho kwenye ufunguo wa gari na kuhakikisha gari nimelifunga kwa usalama. Pamoja na giza lililokuwa limeingia mwangaza toka hoteli hiyo uliniweza kumuangalia Freddy vizuri kabisa akiwa amesimama pembeni yangu. Alinisogelea kama mwana wa mfalme.

“Hi Tina, umependezaaa” alisema huku akiivuta hiyo voweli ya mwisho.
“Asante Freddy” nilimjibu nikifungua mikono yangu kuijibu ya kwake iliyofunguliwa kunipa kumbatio. Kwa sekunde chache miili yetu ilikutana kwa ukaribu ambao haujawahi kutokea. Nilipomuangalia machoni macho yake yalikuwa yanameremeta tena kama nyota usiku. Ni kama alikuwa ananiona hadi chini kabisa ya moyo wangu. Kabla sijasema lolote aliituliza midomo yake kwenye midomo yangu na kuniangushia busu ambalo nusura linifanye magoti yaachie!

Nilipatwa na kizunguzungu cha ghafla kilichonifanya nimng'ang'anie zaidi. Moyo ulinidunda.

Nilikuwa nimevalia gauni la rangi ya nyeusi ambalo lilikuwa na rangi nyekundu inayong'ara ikiwa imetapakaa kama madoa madoa kwa mbele. Rangi hiyo ya madoa madoa iligawanya kifuani na kiunoni kwa rangi nyingine nyeusi. Karibu na magoti lilikuwa linaonesha kidogo ngozi yangu. Nilivaa hereni za rangi nyekundu vile vile. Gauni hilo lilikuwa limefanana kiasi na gauni alilovaa Michella Obama siku ya kutangazwa ushindi wa uchaguzi wa Obama. Tofauti ni kuwa gauni langu lilikuwa ni kipande kimoja tu. Nilivaa viatu virefu kiasi vya rangi nyeusi na mkoba wangu ulikuwa umechanganya rangi nyeusi na nyekundu vile vile. Aliniangalia mara ya pili na kujiuma mdomo kwa tamaa. *Na bado.*

"Duh, haya twende!" alisema akinishika kwa mkono wake wa kushoto kuniongoza kuelekea kwenye gari lake.
Nikiri kwamba sikutarajia kuwa Freddy angeweza kuwa na gari kwani nilimuona ni mmoja wa vijana wabangaizaji tu. Lakini lilikuwepo pale na nilijua halikuwa gari jipya na la kifahari hata kidogo. Ni wazi alikuwa amenunua kwa kuagiza au kutoka kwa madalali hapa hapa Dar. Ilikuwa ni Toyota Mark II ya rangi nyeusi. Sikujali. Kitu kimoja kilichonigusa nilipoingia tu ndani ya ile gari ni usafi. Gari lilikuwa safi na hata lilikuwa ni mtumba ni wazi kuwa Freddy alikuwa analiweka safi. Kwa kweli nilitaka nijue ni lake au la kuazima.

"Gari nzuri Freddy, safi sana" nilisema na kumpa compliment.

"Asante" alijibu huku na yeye akifunga mlango wa upande wake wa dereva baada ya kuzunguka mbele ya gari alipohakikisha mlango wa upande wangu umefungwa.
"Ulinunua wapi?' nilimuuliza kwa udadisi huku nikigeuza kichwa changu kuangalia viti vya nyuma ambako vyote vilikuwa safi kabisa. Harufu yake ilikuwa ni kama lililooshwa kwa sabuni. Nilijisikia bado niko fresh kabisa.
"Yule braza wangu wa pale Hotelini kuna jamaa anawafahamu ndio aliniunganisha nao" aliniambia. Kumbe lilikuwa lake kweli.

Tulichukua barabara ya Nelson Mandela kuelekea nyumbani kwake. Mara baada ya kupita eneo la Hosteli ya Mabibo tuliendelea mbele hadi karibu na barabara ya Kigogo ambapo tulikata kulia kuelekea Tabata. Giza lilikuwa limeshaanza kuingia na kusema ukweli nilikuwa katika huruma yake tu kwani sikuweza kujua mitaa ya huko ikoje na nilitamani ningeenda ikiwa mchana ili hata ikinibidi kukimbia nijue pa kuanzia. Nilimuamini Freddy.

Alikuwa anaendesha taratibu huku tukizungumza mambo mbalimbali ya maisha na hasa ubovu wa barabara, mpangilio wa nyumba na kukosekana kwa alama za kueleweka za barabarani. Ilitukuchukua karibu dakika arobaini na tano kuweza kufika nyumbani kwake ambapo niliweza kutambua baadaye kuwa ilikuwa ni karibu zaidi na Kinyerezi na pembezoni mwa Segerea. Alikuwa anaishi ndani sana huko. Miaka michache tu iliyopita maeneo hayo yote yalikuwa ni matupu tu lakini miaka ya karibuni watu wengi wa kima cha kati wamejenga huko. Tulipofika nyumbani kwake aliniacha ndani ya gari na kwenda kufungua geti la nyumba yake.

“Hapa ndio ninapopanga Tina” alisema na hivyo kunijulisha kuwa hiyo haikuwa nyumba yake hasa bali alikuwa ni mpangaji. Alirudi kwenye gari na kuliingiza gari ndani. Hakukuwa na mtu yeyote wala walinzi ila ulinzi ulikuwepo kwani nilisikia mbwa wakibweka kutoka nyuma ya nyumba ambako niliweza kuona kibanda chao.
“Wadogo zako na mtoto hawapo?” nilimuuliza kwani nilikuwa najiuliza itakuwaje hapo au nitafanya nini nikikutana nao na maswali mengine kem kem. Lakini ukimya wa hapo nyumbani ulinihakikishia kuwa hawakupo. *Labda watarudi baadaye.*
“Hapana wameondoka kwenda kwa Tall” alinijibu huku akianza kufungua mlango wa mbele wa nyumba yake. Taa ya uwani ilikuwa inatumilia na gauni langu lilikuwa linang’ara.

Kwa nje nyumba yake ilikuwa ni ya kawaida kabisa iliyopigwa rangi nzuri ya kahawia kidogo. Madirisha yake yalikuwa yamewekwa senyenge za kashata kashata na ilikuwa ni ya ukubwa kiasi. Niliweza kuona kwenye kona ya kushoto karibu na ukuta kulikuwa na tangi kubwa la SIMS ambalo ni wazi lilikuwa linakusanya maji. Chini ya tangi kulikuwa pampu ya maji ambayo ilikuwa imefungwa kwenye kitu ambacho naweza kusema kuwa ni kama kabati la chuma hivi.

Mlango ulifunguka na akanikaribisha ndani. Kama nikisema kuwa nyumba ilikuwa safi ndani mnaweza kusema natia chumvi. Kwanza sikuweza kuamini kuwa ndani ya nyumba hiyo anaishi zaidi ya mtu mmoja na miongoni mwao ni mtoto mdogo. Kila kitu kilikuwa kimepangwa vizuri kabisa. Sebule ilikuwa upande wa kulia ambayo ilikuwa imepangwa safu ya makochi makubwa ya ngozi nyeusi inayong’ara. Sehemu ya kulia ilikuwa nyuma kidogo tu makochi na kati yake walitenganishwa na jikoni. Upande wa kushoto kulikuwa na safu nyingine ya sebule kitu ambacho kilikuwa ni cha tofauti. Ni wazi kulikuwa na sebule ya wageni na ya wenye nyumba. Sebule ya wageni ndiyo ilikuwa imepangwa utadhani ni hoteli ya kitalii kwani karibu kila kitu kilikuwa cha hadhi ya juu kabisa. Ukutani upande huo kulikuwa na kabati kubwa la vioo ambamo niliweza kuona kutoka niliposimama vyombo mbalimbali vya kulia na kunywea vikiwa vimepangwa kwa aina ya matumizi yake. I was *impressed.*

“Karibu Tina” aliniambia akiniekeleza kuelekea kukaa kwenye sebule ya wageni.
Niliingia na kuketi kwenye seti hii ya sofa ambayo upande huu wa wageni ilikuwa ni rangi ya pembe za ndovu. Mbele yangu kulikuwa na TV ikiwa imewekwa beneti kabisa na radio kubwa ya kisasa na kabati dogo la kuweka CDs na DVDs. Niliangalia juu na kuona pangaboi ambalo lilikuwa limetulia. Kulikuwa na badiri zuri humo ndani ambalo ilikuwa ni ishara kuwa mitambo yake ya AC inafanya kazi. Huyu kijana vipi? Nilijiuliza.

Freddy wa kwenye nyumba hii siyo kijana yule mwenye kibanda chake cha kubangaiza katikati ya mji. Nilitamani nianze kumhoji maswali ili anidadavulie kwa undani kwanini ni kama nilikuwa nakutana na mtu mwingine tofauti kabisa. Aliniacha hapo na kwenda ndani chumbani kwake ambako alibadilisha na kurudi akiwa amevaa kaptula ndefu ya rangi nyeusi na tsheti ya rangi ya bluu. Alikuwa amezivuta nywele zake nyuma na kuzifunga kwa pamoja. Alikuja kukaa nami.

Mwili ulikuwa unanitetemeka. Kulikuwa na kimya cha ajabu kwani ukuta uliozunguka nyumba na jinsi nyumba ilivyojengwa kulikuwa kumetengeneza uzio wa sauti (sound barrier) ambayo ilifanya kelele za nje kutosikika ndani kabisa. Aliniomba nimfuate anioneshe 'jiografia' ya nyumba ili nikitaka kitu nisianze kuuliza wapi ni wapi. Kutoka kwenye sebule zile mbili kuna kabati la ukutani ambako unaweza kutundika makoti n.k na chumba cha pili ambacho kinapakana na jikoni aliniambia ni kama kaofisi kashughuli zake. Ilifuatia seti ya bafu na choo cha jumla na upande wa kulia kulikuwa na stoo ya vitu mbalimbali. Upande huo huo kulilikuwa na chumba cha kwanza cha watoto ambacho kilipakana na chumba kingine (vikiangaliana) ambacho kilikuwa cha mdogo wake wa kiume. Kilifuatia chumba kikubwa cha wageni ambacho ndani kilikuwa na bafu na choo chake na upande wa mwisho ni chumba kikuu. Ukitoka sebuleni unaweza kuona mlango wa chumba kikuu (masterbedroom) ukikuangalia kama unakuita. Nje yake kulikuwa na pazia.

Sebule yake ya wageni ilipambwa vizuri ikiwa na maua kwenye kona zote mbili zilizo pembeni ya TV yake, kulikuwa na carpet kubwa la rangi rangi za nyeupe na nyeusi la sufu ambalo lilifanya miguu iwe kama unatembea kwenye mawingu hivi. Kati ya kochi ambalo nilikaa awali na TV kulikuwa na meza nzuri ya kigoo iliyokuwa imewekwa huu ya kasa wa kuchonga. Pembeni ya sofa na kochi jingine kulikuwa na meza ndogo ndogo za kigoo ambazo nazo zilikuwa migongoni mwa kasa wadogo. Upande wa kulia ukiangalia TV kulikuwa na dirisha kubwa ambalo lilikuwa limefunikwa na mapazia ya kupendeza ya rangi ya maziwa vile vile. Upande mmoja wa dirisha kulikuwa na picha kubwa ya kuchora mwanamke wa kimasai akiwa anacheka na kufanya kila ukiangalia hiyo picha na wewe unajisikia kutabasamu.

Kwenye ukuta nyuma ya TV kulikuwa na sanamu mbili zilizokuwa upande huu na upande huu – mmoja mwanamke na nyingine mwanamme. Na kati kati ya hizo picha kulikuwa na picha kubwa ya Mfalme Selassie akiwa juu ya farasi mweupe ambaye alikuwa ametandazwa juu yake kitambaa cha rangi ya dhahabu. Mfalme mwenyewe alikuwa amevaa mavazi yake ya kijeshi ya wakati wa sherehe na kofia kubwa iliyokuwa na manyoya ya rangi nyekundu yaliyoelekezwa kwa nyuma hivi. Mfalme alikuwa ameinua kichwa chake upande hivi kama anaangalia mbali hivi. Chini kulikuwa na maneno "Simba wa Yuda". Niliipenda picha ile.

Wakati naangalia picha hiyo nilikuwa nimesharudi na kuketi huku viatu vyangu nikiwa nimevivua na kuviweka kwenye kabati. Nilijisikia niko nyumbani.

"Niwashe TV wakati naandaa chakula?" aliniuliza.
"Unaanza kupika?" niliuliza kwa tahamaki kwani nilitaka akae pembeni yangu tuzungumze na kufahamiana zaidi na zaidi. Halafu hilo wazo la yeye kuingia jikoni kwa kweli sikulipenda.
"Hapana nilishapika nataka nipashe moto tu." Alinijibu. Alipitisha mkono wake juu ya kichwa changu na kuuteremsha taratibu kufuata paji la uso wangu hadi kidevuni. Sikuelewa ni nini lakini lijisikia raha. Nusura niung'ate.
"Naweza kukusaidia kupasha bwana" nilisema huku nikiamka. Na yeye aliniongoza kuelekea jikoni.

Haikuchukua muda niliwezakupasha vitu ambavyo ni wazi vilikuwa vimeandaliwa vizuri jioni hiyo. Kumbe ningeahirisha kwenda hapo nadhani kuna vitu *vingedoda.*
“Umepika saa ngapi” nilimuuliza kwa udadisi kwani amezidi kunishangaza.
“Niwe mkweli, Uncle Tall alikuwa hapa kunisaidia” alisema na wote kwa pamoja tukacheka. Kumbe walikuwa wanajua ana ugeni siku hiyo. Nikamheshimu Tall vile vile. Kwa ajili ya watu wawili chakula kilikuwa ni kingi mno. Kama ndio ilikuwa ni tafrija ya muungano kwa hakika tulihitaji watu wa kutuunga mkono. Kama dakika kumi na tano hivi chakula kilikuwa tayari mezani, pilau, kuku wa kukaanga, sambusa, mchicha wa kuchemsha, matunda na glasi za Dodoma wine. Vyakula vingine kwa kweli nilimuambia aviache tu waje kula watoto kesho tusije tukakafuru bure.

Tulipoketi mezani kula aliniangalia machoni na kutabasamu. Alimimina glasi za mvinyo kama nusu tu hivi kwa kila glasi. Harufu nzuri ya Dodoma wine ilipenya kwenye matundu ya pua yangu na kunipa raha safi. Kwa wanaojua wine ni mojawapo ya wine nzuri kabisa kutoka katika bara la Afrika na inasifika katika sehemu mbalimbali duniani kama ni mojawapo ya wine bora sana duniani. Tulinyanyua glasi.
“Clementina, kuanzia leo na milele umenipa furaha, tunywe kwa afya na mafanikio. Kwa mimi na wewe” alisema.

“Kwa mimi na wewe” nilimjibu. Tukazigonganisha.
Tulianza kula taratibu huku tukizungumza na kupigishana soga. Lakini kwa muda mrefu tulikuwa kimya na tunaangaliana na kutabasamu. Kama kungekuwa na uwezo wa mtu kujua mawazo ya mtu mwingine basi wakati ule kwa kweli tungekamatwa kwa mawazo ya uhalifu. Nilikuwa nashindwa kumuangalia machoni kwa muda mrefu; kila ninapoangalia nilikuwa natamani nimguse. *Ee mola yamenikuta nini mimi.*

Tulipomaliza kula nilimsaidia kutoa vyombo mezani na kama nilivyotarajia akaanza kuviosha mara moja. Sikumuacha avioshe mbele yangu. Nilimuambia afanye jambo jingine miye nitaviosha. Kusema kweli ilibidi nijicheke kwani sikumbuki mara ya mwisho kuosha vyombo ilikuwa lini. Lakini mtoto wa kike nimelelewa vizuri sikutahiji kukumbushwa au kupewa semina. Haikunichukua muda nilikuwa nimemaliza kuosha vyombo vyote, kuvisuuza na kukausha. Akaja kunisaidia kuvirudisha sehemu zake kwenye kabati. Mara moja jiko na dining area vyote vilikuwa safi tena. *Kaka msafi!*

Tukarudi sebuleni kuketi na tukaendelea na soga mbalimbali huku chakula kikishuka taratibu. Mvinyo tulioanza nao mezani tulikuwa tumeuleta kwenye ile meza ya kioo na kwa pamoja tukawa tunakunywa taratibu huku tunacheka. Tulikuwa kama marafiki ambao tumekutana baada ya miaka mingi. Mbele yake kwa kweli nilikuwa nimetulia na nimefika. Moyo wangu ulikuwa hauna wasiwasi tena. Nilikuwa kama ndege aliyenaswa na hatimaye alijua kuwa amenaswa na hivyo juhudi zozote za kujinasua hazikuwa na sababu. Alisubiri kuwa kitoweo.

“Unajua kucheza muziki?” aliniuliza baada ya ukimya wa sekunde chache. Nusura nimpe jibu la Kiswahili, “unauliza kata kisimani” au lile maarufu la mtu kuuliza “Biblia kanisani” au “tasbihi kwa shehe”. Aliniuliza kama najua kucheza muziki.
“Si sana” nilimjibu kwa haya za kike. *Angejua.*

“Muziki gani unapenda” aliniuliza akiwa amesimama karibu na CD player yake iliyokuwa pembeni na TV. Kulikuwa na mkusanyiko wa CDs nyingi sana zikiwa zimepangwa kwa namna ya mtindo wa muziki kuanzia RnB, Jazz, Ndombolo, Blues, Zilipendwa, na Reggae. Sehemu ya Reggae ndiyo ilikuwa na CDs nyingi kweli.
“Wewe chagua tu” nilimuambia bila kujaribu *kumuweka* mtegoni.
“mmh, huu sasa mtego” kumbe aliuona mtego; akakubali kunasa.

Aliangalia kwenye nyimbo za kicongo. Akaniomba nisimame nicheze naye. Nilipoanza kuinuka ndiyo muziki ukaanza kuunguruma. *Yesu na Maria!* Mwanzoni sikuwa nimeona spika zilikuwa wapi. Lakini Freddy alifanya mambo ya ajabu, Spika zilikuwa zimefichwa kwenye kuta mbele, kwenye dari juu na kuta za nyuma. Sauti ya bezi ilikuwa inatoka chini sakafuni. Sebule ilikuwa imezungukwa na sauti ukichujwa safi kabisa. Alikuwa ni Mbilia Bell akiwa na Tabu Ley wakiwa Afriso International, wimbo haukuwa mwingine bali wa enzi za TP-OK Jazz, *Mario.* Nilijipeleka mwenyewe mikononi mwake kama mbwa mdomoni mwa chatu.

Mkono wake wa kulia uliufunga mkono wangu wa kushoto juu ya mabega yetu. Niliweka mkono wangu wa kulia kwenye bega lake la kushoto. Mkono wake wa kushoto ulikuwa umezunguka nusu ya kiuno changu. Toleo la Mario yakina Mbilia Bel ukilinganisha na kina Franco ni kuwa toleo lao lilikuwa ni la taratibu kidogo katika mapigo yake. Tulianza kunesa nesa kwa pamoja. Nilijisikie raha mikononi mwake. Alinibusu nikarudisha taratibu. Moyo ulikuwa unanidunda. Aliniachilia na kunizungusha kwa mkono wake wa kulia na kunivuta karibu, nikanasa kama ufunguo kwenye kitasa. Sebule ilianza kuwa ndogo.

Mario ilipoisha tu akaingia tena Mbilia Bel na wimbo mwingine wa Tabu Ley *Beyanga.* Huo wimbo nilikuwa naupenda sana kwani ulikuwa unanigusa sana.

Na Silika nakozoi eloko nini e
Na tomboka nakozoi reponse nini o
Moto soko akoli na ezaleli banda na bomwana naye
Akoki kosilisa na mokolo moke te tika a sala
Na ko swana swana se pamba, ezali motindo na ye
Na ndimaka te nalingi ye, ebongi na vanda na ngai
Libala oyo ba mbanda bipayi binso
Nakotisi moto na singa, epayi pasi o
Nazali na etombo na motema kasi nalingi se ye
Akoki kosala na silika soki abimeli ngai
Na kozanga liloba na pesa ye, na bandi nde kolula ye!

Duh.. alivyokuwa akilalamika alikuwa ananifanya natamani kulia; sijui kama Freddy alikuwa anajua wimbo unamaanisha nini. Joto lilizidi kunipanda. Pamoja na AC kufanya kazi yake vizuri bado joto lilizidi kuongezeka. Kama vile alijua ninavyojisikia aliniachilia kidogo.

“Unataka maji ya kunywa” aliniuliza, nilimkatalia. Nilichukua glasi ya mwisho ya mvinyo nikaigigida. Nilianza kujisikia ukichaa wa aina fulani.
Wimbo ulipokaribia kwisha nikamuuliza kama anazo mojawapo ya nyimbo maarufu za Kiswahili zilizopendwa.

Aliniambia anao. Akaenda na kuitafuta CD na kuiweka. Gitaa lilianza kuzungumza.

Oh Georgina, siku uliyoondoka
Uliniacha nalia na machozi
Umekwenda kuishi mbali nami
Georgina wa mama

Duh! Kilipofika kibwagizo huku sauti ya Marijani ikinung'unika nilishindwa kujizuia. Niligeuka na kumpa mgongo na kuanzakucheza kwa kukatika nikijizungusha mbele yake kabisa. Nilijisikia kusisimka nilivyokuwa namgusa kiuchokozi. Wimbo ulipokwisha nilikuwa nimetota kwa jasho na *mengine.* Wote wawili tulikuwa tunahema. Kabla sijatulia CD nyingine ikapokea. Alikuwa ni Brian McKnight akiwa na "Back at One". Alinivuta tena karibu yake, tulikuwa tunatoka jasho. Safari hii nilizungusha mikono yangu kwenye shingo yake kabisa, ya kwake ilikuwa kiunoni kwangu; nililaza kichwa changu shingoni kwake. Nilimbusu. *Oh malaika nisaidieni.* Brian alinung'unika na kuelezea hasa kilichokuwa moyoni mwangu. Niliombea ndicho kilichokuwa moyoni mwa Freddy, mjamaika wangu.

It's undeniable... that we should be together...
It's unbelievable how I used to say that I'd fall never
The basis is need to know, if you don't know just how I feel,
Then let me show you now that I'm for real...
If all things in time, time will reveal...
Yeah...

One... you're like a dream come true...
Two... just wanna be with you...
Three... girl it's plain to see... that your the only one for me...
Four... repeat steps one through three...
Five... make you fall in love with me...
If ever I believe my work is done... then I start Back at One (yeah)

So Incredible... the way things work themselves out...
And all emotional, once you know what it's all about babe...
And undesirable... for us to be apart...
Never would of made it very far...
Cause you know that you've got the keys to my heart
Cause.

Wimbo uliendelea hadi mwisho. Ulipofika mwisho nilikuwa nimelowa na machozi ya furaha.
"Unalia nini babe" aliniuliza akinisogeza mbele yake kuniangalia machoni.
"nothing" nilimjibu kwa kiingereza.

Kutoka hapo akaweka wimbo mwingine ambao kwa kweli aliniambia kuwa ni *dedicated* kwangu. Wimbo ambao unatajwa kuwa ni miongoni mwa nyimbo nzuri kabisa za mapenzi. Ulikuwa ni wimbo wa Boyz II Men uitwao "I'll make Love to you". Sauti za waimbaji zilikuwa ni burudani tosha. Ni miongoni mwa nyimbo za Babyface ambayo inapendwa sana na ni zawadi kwa wale wote wapendan. Niliyasikiliza maneno yake tukiwa tumekumbatiana. Freddy alikuwa anaimba kwa kunong'oneza kwenye masikio yangu.

Close your eyes, make a wish

And blow out the candlelight
For tonight it is your night
We're gonna celebrate, all through the night
Pour the wine, light the fire
Girl your wish is my command
my submit to your demands
I will do anything, girl you need only ask

(Chorus)
I'll make love to you
Like you want me to
And I'll hold you tight
Baby all through the night
I'll make love to you
When you want me to
And I will not let go
'Till you tell me to

Girl relax, let's go slow
I ain't got nowhere to go
I'm just gon' concentrate on you
Girl are you ready, it's gon' be a long night
Throw your clothes (throw yoor clotes) on the floor (on the flore)
I'm gonna take my clothes off too
I've made plans to be with you
Girl whatever you ask me, you know I can do

(Chorus)

Baby tonight is your night
And I will do you right
Just make a wish on your night
Anything that you ask
I will give you the love of your life, your life, your life

Wimbo huo ulipofika tamati nilikuwa nimeishiwa nguvu. Nilikuwa nashindwa hata kutembea; nilikuwa niko wima kwa sekunde chache mikononi mwake kama sungura aliyenasa kwenye sanamu iliyotiwa gundi. Kijasho cha baridi nilikikisia kikitiririka kwenye kwapa zangu.

“Naona uko chepe kabisa” aliniangalia kwani uso wangu ulikuwa umeloa jasho na kuharibu make up yangu.
“Hata wewe mbona” nilimjibu wote tukacheka.
“Unataka tukaoge mpenzi maana hili jasho?” alisema. Hata asingeniuliza nilikuwa na mpango wa kwenda kujimwagia maji kidogo maana moto alioawasha ingekuwa *murder case* kama nisingejituliza kidogo. Alinitangulia kuelekea chumbani kwake ambako kulikuwa na bafu na choo vilevile.

Alipofungua mlango nusura nizimie. Kama kile kilikuwa ndiyo chumba cha maajabu basi mwenzenu nilishangaa. Kwanza kilikuwa kikubwa kuliko nilivyofikiria; ni kikubwa. Kitanda kilikuwa katikati kabisa. En*eo la mauaji.* Kulikuwa na meza na kioo upande wa kulia karibu na dirisha, upande wa kushoto kulikuwa na mlango wa kuingia msalani. Zuria lake lilifanana na lile la sebuleni. Taa mbili zilisimama kama walinzi na mashuhuda pembezoni mwa kitanda. Kulikuwa na harufu nzuri chumbani humo. Vingine vilivyokuwepo kwa kweli inatosha kabisa kuandika kitabu cha mapambo ya nyumba. Udadisi juu ya Freddy ulinizidia.

Alinielekeza bafuni. Niliweka mkoba wangu juu ya kitanda na kufungua mlango wa bafu. Kama kilivyokuwa chumba bafu lake lilikuwa kubwa, likitenganishwa upande mmoja wa kulia choo, katikati kulikuwa na sinki la kunawia na kushoto kulikuwa na sinki la kuogea la mviringo. Niliangalia yalipo mataulo nilichukua muda na kujifunga kichwani kwanza. Nilifungua vifungo vya gauni langu ambavyo vilikuwa vimeanza shingoni hadi chini kwa mbele. Nililitundika kwenye mojawapo ya pini za kutundikia nguo. Nilipomaliza kuvua nguo zote niliingia kwenye sinki; nilifungulia maji ya mvua. Aah safi kabisa. Maji yalianza kutiririka mgongoni kwangu huku nikijipaka sabuni taratibu.

Nilikuwa nimeweka sabuni machoni, nilipohisi mtu mwingine kaingia kwenye sinki.

“Freddy” niliita.
“Naam mpenzi” aliniitikia. Nilipangusa kwa haraka macho yangu ili nimuone. Alikuwa uchi wa mnyama mbele yangu.
“Nikusaidie kukusugua” aliniuliza huku akininyang’anya kitaulo kidogo nilichokuwa nimekishika mkononi. Ningeweza vipi kukataa wakati kwa kweli nilikuwa chini ya huruma yake? Maji yakaanza kummwagikia na yeye nilijiosha uso wangu ili nimuangalie kwa sekunde. Nilitabasamu. Kwa kweli ilikuwa ni kama kwenye movie nzuri. Freddy sikuwa nimesema mapema alikuwa na weusi ule wa kung’ara yaani kama ni Mmandingo basi alikuwa ni kweli mmandingo. Sasa maji yalipommwagikia vile na mikono yake pamoja na misuli yake vyote vilimfanya aonekane kama supa modo fulani hivi. Nilijisikia kusisimka zaidi.

Taratibu aliongeza sabuni kwenye kile kitaulo. Akaanza kunisugua taratibu. Nikaamua kumgeuzia mgongo maana aibu zilinizidi kumuangalia machoni. Kama fundi mtandaza marumaru kwenye kuta za kasri la mfalme Haroun Bin Rashid mikono yake ilipitisha taulo mgongoni kwangu katika mizunguko ya taratibu akienda kulia na kushoto kuanzia shingoni na taratibu kuelekea kiunoni. Nilikuwa nimeegemeza mikono yangu chini ya bomba la maji ya mvua huko kichwa nimekiepesha kisiangukiwe na maji. Mchuruziko wa maji mgongonano na mguso wa mikono yake ulinifanya nizidi kuhema. Alipofika mapajani nilishindwa kuotea atafanya nini; niliombea afanye nilichotarajia. *Hakufanya.*

Niligeuka kumtazama, nilipunguza nguvu ya maji ikawa inanipiga mgongoni taratibu. Alianza kunisugua kwa mbele. Matiti yangu yalikuwa yanapwitapwita kwa hamasa. Alitumia mkono wake mmoja kuyasugua taratibu huku mkono wenye taulo ukinipaka sabuni. Nilifumba macho. Aliendelea kufanya hivyo huku nimejiuma meno yangu kwa utamu. Safari hii hakukopesha, mkono wake uliokuwa hauna taulo aliuleta hadi kwenye waridi langu lililokuwa limetota kwa zaidi ya maji ya bombani. Akaupitisha juu juu tu kiuchokozi! Niliguna na kuyafumbua macho yangu.

“Freddy!” niliita na kubana miguu yangu.
“Tina” aliniita na kuuchomoa mkono wake na katika kufanya hivyo aligusa kwa juu mbegu ile iguswayo! Ingekuwa sehemu nyingine ningemrukia! Alinigeuza na kuja upande wa bomba la maji ili ajimwagie kujisafisha zaidi zaidi. Ilikuwa zamu yangu kumnyang’anya taulo. *Tate nane.* Yeye alitulia kama sanamu

ya Michaengelo iliyochongwa kiufundi. Macho yetu yalipogongana tulitabasamu. Nilianza kumsugua taratibu kifuani na kwa mkono mmoja nilikuwa nampampasa sehemu mbalimbali mwilini. Jamani mwili wake ulikuwa ni kama sumaku, nilikuwa nimenaswa na sikutaka kuuachia kabisa. Nilitumia mkono wangu wa kulia kuanza kumsugua mfalme wa hekalu langu aliyekuwa amesimama katika utayari wa kutoa ushirikiano wa kuyafungua malango ya kasri langu. Freddy aliguna kwa raha. Nilimsugua taratibu huko nikiacha maji yamuangukie yakiwa na mapovu ya sabuni.

Nilitamani nimmeze hadi kooni, *literally!*

Nilimmwagia maji na kumsuuza tena na tena, alipendeza. Nikaanza kupiga magoti bafuni niweze kumuonja kama ni mtamu jinsi anavyoonekana au ndiyo utamu wa kuona tu. Freddy alifumbua macho.
“ooh no” alisema
“Nini jamani mpenzi” nilimuulize nikiwa tayari nimefungua kinywa changu kuona utamu wa mshikaki uliowiva.
“Bado darling, bado” aliniambia nakuniinua. Nilijisikia kukataliwa na kunyimwa “haki yangu”. Nilitamani niwe na bango nianza kuandamana kudai haki ya kumpa raha ambayo sijampa mtu mwingine katika maisha yangu.
“Bado nini, mbona uko tayari” nilimuambia kwa kulalamika.

“Haraka haraka hun, haina baraka” aliniasa. Sikuelewa. Niliponyanyuka alinivuta karibu yake na kunikumbatia huku miili yetu ikiwa imeloa maji chepe chepe, alianza kunibusu taratibu, busu juu ya busu, lilikuwa ni busu la ukame, busu la njaa, busu la usongo! Nilirudisha la kwangu. Aliponiachilia midomo yake ikaanguka kwenye matiti yangu ambayo chuchu zake zilikuwa zimetuna *kwa umoja, amani, utulivu na mshikamano* wa mahaba! Alifyonza moja baada ya nyingine, huku vidole vyake vikiwa vinanisalimia taratibu kunako. Sikubana miguu yangu tena. Nilimuachia afanye atakalo, kwa hakika alilifanya. Ukichanganya mabusu na kunyonywa chuchu pamoja na kuchezewa kwenye waridi langu nilijisikia kuchanganyikiwa hadi kisogoni.

“Unanimaliza Freddy” nilifanikiwa kusema kabla hajanifunga mdomo wangu kwa busu jingine motomoto.
“Unataka niache?” alihoji huku akijua jibu lake. Ilibidi nimhakikishie.
“Usiache jamani” nilinung’unika.

Tulichezeana kwa muda bafuni hapo na kabla hatujaamua kumalizana kabisa kwani nilikuwa hoi bin taaban alifunga bomba na kuyakatisha maji yasiendelee kutiririka. Sijui kama lile tanki la Sims lilikuwa bado na maji! Tulipotoka bafuni alinisaidia kunipangusa kwa taulo safi la rangi ya samawati ambalo lilikuwa laini kumfaa mtoto mchanga. Baada ya kujifungua taulo nililiokuwa nimejifunga kichwani na kujikausha nilimgeukia na bila ya yeye kutarajia nilimsogelea na kumpa ulimi wangu tena. Miili yetu ilikuwa imekauka lakini sehemu nyingine za mwili wangu zilikuwa bado zinazidi kutota na kuloa kabisa. Tulianza kupelekana kitandani huku tukiwa tunapapasana na kutomasana huku ndimi zetu zikiwa zinapigishana sarakasi. *Tamu ya utamu!*

Nilijiangusha kwa nyuma kitandani nikimvuta aje juu yangu. Alinifuata. Alinisogeza katikati ya kitanda kabisa, alikuwa juu

yangu akiendelea kunibusu na mimi nikirudisha mashambulizi. Hadi wakati huo nilikuwa nina uhakika kuwa ngoma ilikuwa droo. Aliniachilia na kuinuka taratibu. Sikutaka aniachilie.

“Ah.. Freddy unaenda wapi tena” nilimbembeleza asiondoke.
“Siendi mahali mpenzi, subiri” aliniambia nisubiri kidogo aliondoka chumbani akiuacha mlango ukiwa wazi kidogo. Nilikuwa nimelala chali katika suti yangu niliyokuja nayo duniani. Mtoto wa kike nilikuwa nimejilaza kwenye kitanda cha Freddy! Wiki moja kabla sikujua kuna mtu anaitwa Freddy! Ndani ya wiki moja nilikuwa nimelazwa kama kuku aliyewekwa kwenye kibanio akiwa tayari kuongezwa ndimu na chumvi, pili pili na limau! Mwanga hafifu wa chumbani humo ulinifanya niwe kama ninayemulikwa na mbalamwezi juu ya kilima cha mawe pembezoni mwa bahari ya Hindi. Nilitaka arudi na kuja kumalizia alichoanzisha. Nilipitisha mkono kwenye ua langu taratibu. Toba yarabi, *I’m so ready* nilijiambia.

Alirudi mkononi akiwa na chupa ya asali. Aliiweka pembeni mwa kitanda. Ya nini tena hii nilijiuliza. Hakutulia bali alikwenda kwenye kabati lake la nguo ambapo kwa sekunde moja tu alirudi na tai ya rangi nyekundu mkononi mwake. Hapa pana kazi, nilijisemea tena.
“Unaniamini Tina” aliniuliza akija juu ya kitanda juu yangu.
“Kabisa Freddy” nilimjibu hata bila ya kusita. Yaani hadi wakati ule alikuwa hajui ninamuamini?
“Asante” alinijibu. Alinishika mikono yangu na kuniinua nikae. Sikutaka kwani nilitaka niendelee kulale aje na kumaliza *alichokianzisha.* Hata hivyo nilikubali. Nilikuwa tayari kwa lolote kutoka kwake. Alichukua ile tai na kuniambia atanifunga macho kabisa. Hii ilikuwa *first* kwangu.
“Unanifunga ili kiwe nini” nilimuuliza. Kwanini hakutaka nione. Nilianza kuingiwa na wasiwasi, sikujua kwanini alitaka kunifunga tu macho.
“Usiogope, niamini tu mpenzi” aliniambia na kunimwagia busu. Nililainika. Alizungusha sehemu pana ya tai mbele ya macho yangu niliyoyafumba na kuifunga nyuma kisogoni. Aliniuliza kama niliweza kuona nilimuambia siwezi kabisa. Alimalizia kwa kusema “safi”. Alinisukuma taratibu kujilaza tena chali.

Mojawapo ya kitu ambacho kilitokea mara moja ni kuwa hisia zangu nyingine zote zikapata nguvu zaidi. Hisia za mguso ziliongezeka, masikio yalikuwa sikivu zaidi, harufu ndio kabisa. Ilikuwa ni kama mtu ambaye amehamisha nishati kutoka sehemu moja ya umeme na kupeleka sehemu nyingine na kusababisha sehemu hiyo nyingine kuwa na nguvu kubwa. Japo nilikuwa siwezi kuona niliweza kuhisi kila kitu kilichokuwepo humo chumbani. Nilijilaza chali kabisa kwa urefu wangu wote. Freddy alikuwa kimya.
Kilichonishtua nusura niruke ilikuwa ni mchirizi wa kitu laini ukipita kuanzia kwenye paji la uso, pua, midomo, shingoni, kifuani kitovuni, kiunoni hadi katikati kabisa utadhani mstari wa Greenwich na kugawa kuta zangu upande wa mashariki na magharibi kama dunia inavyokatwa na mistari ya longitudo. Nilitoa ulimi wangu kulamba kujua ni nini. *Asali.* Nilitulia kabisa kama niliyewekwa meza ya upasuaji na daktari bingwa huku nikiachwa kusikilizia maumivu yote ya utamu.

Kabla sijajua anataka kufanya nini, mchirizi mwingine ulianza kudondoshwa juu yangu kuanzia bega la kulia, ukapita juu ya titi langu la kulia nikiusikilizia ukienda taratibu hadi kiunoni na moja kwa moja hadi kwenye vidole vya miguu yangu. Niliweza kuhisi kila tone lilivyodondoka kwenye ngozi yangu. Nilisubiria upande wa kushoto; alifanya hivyo hivyo tena hadi kwenye vidole vya mguu wangu wa kushoto. Sasa kinafuata nini jamani nilijiuliza.

Katika mawazo yangu yote nilihisi atakakoanzia. Labda atanibusu kwanza, au ataanza kuninyonya chuchu na kulamba asali ambayo imezifunika utadhani barafu itamanishayo juu ya mlima Kilimanjaro. Labda ataanza kulamba kwenye waridi langu ambalo tayari lilikuwa na maziwa yakitiririka kama nchi ya ahadi ile Sayuni ya kale. Ndipo nilipogundua kuwa alikuwa kimya kabisa. Sijui alikuw anafanya nini. Sikujua ataanzia wapi, vipi na namna gani. Nilitamani niifungue ile tai niweze kumuona anachokusudia kufanya. Mwili wangu ulikuwa umesisimkwa kupita nilivyodhania inawezekana mwili wa mwanamke kusisimkwa. Nilianza kuhesabu kimoyomoyo wapi ataanzaia *Ataanzia wapi.*

Dole gumba!

Kati ya viungo vyote vya mwili wangu ambavyo angeanza kunipa raha sikutarajia kuwa ingekuwa dole gumba la mguu wa kulia. Nusura niunyanyue mguu kwa nguvu na kuvunja taya la mtu. Niliendelea kutulia kama maji mtungini na kama mtu akinyolewa nilijiachilia katika kiwembe chake. Ulimi wake ulianza kufuata mchiriziko wa asali kuelekea juu kiunoni kwangu, mikono yake ilikuwa inanipapasa kwa wakati mmoja mchanganyiko wa joto la mwili na mguso wa vidole vyake vilinifanya nusura nizimie kwa mahaba. Aliendelea kuja juu kwa ulimi wake na alifika hadi kwenye matiti na kama mtu aliyekuwa na njaa kali alianza kuyabugia moja baada ya jingine kwa kupokezana. Aliilamba asali kwenye chuchu zangu na moja kwa moja akaja kunipa busu tamu mdomoni, tamu tamu kama sukari; *i'm serious!*

Akaja juu yangu kabisa na kuanza kurudi kwa kuanzia juu sasa, Alianza kubusu kila nchi na kona ya mwili wangu. Mikono yangu ikiwa imeachiliwa upande huu na upande ule wa kitanda nilikuwa kama ile picha ya Da Vinci ya *Mtu.* Alinibusu na kunilamba na vidole vyake vilikuwa vinanivinjari. Nilibakia kunung'unika kwa mguno wa raha na furaha. Aliyarudia tena matiti yangu akiwa katika safari yake ya kwenda huko kuliko. Akapokezana chuchu-midomo, midomo-chuchu – *hii ndima.* Katika vitu vyote ambavyo sikutarajia katika maisha yangu yote ya mapenzi ni pale ulimi wake ulipoenda na kubusu na kulamba hadi kwapa zangu! Alilamba za upande wote na kuning'ata kidogo, na kurudi tena kwenye chuchu-sijui alikuwa anafanya utafiti?

Nilikuwa nimelegea kabisa, nilikuwa sina nguvu hata ya kusema, nilikuwa nakatikakatika kitandani hapo na kujizungusha utadhani naendeshwa na mashine fulani hivi. Wakati huo wote wimbo wa Barry White "I wanna lay you down" ulikuwa unatusindikiza. Nilikuwa ninasikia raha ya kila namna, raha iliyopita mfano, raha mara milioni moja na zaidi ya raha niliyowahi kupata katika mapenzi. Machozi yalianza kunitiririka taratibu yakiangukia kwenye mto niliokuwa

nimeegemeza kichwa changu. Yalikuwa ni machozi ya raha na utamu. *Huyu kijana nimemtafuta wa nini miye.*

Nikiwa najisikilizia hivyo, Freddy alikuwa anarudi chini taratibu, akautumbukiza ulimi wake kidogo kwenye kitovu na kuzungusha kwa raha. Niliinyanua mikono yangu.
“Jamani Freddy” nilifanikiwa kutoa sauti.
Hakusema kitu.

Alifika kwenye kiuno changu kati ya mpanga wa tumbo na malango ya utukufu. Aliichanua miguu yangu. Mama yangu. Sijui atafanya au hafanyi, atafanya au hafanyi, sijui atafanya au hafanyi – toba anafanya! Ulimi wake ulipita kwenye waridi langu na kuchanua kuta zake zilizokuwa zimefura kwa kujawa na damu ya msisimko.
“Aaaaaah!” ndio sauti pekee niliyofanikiwa kuitoa. Kabla sijatulia tena akauridisha ulimi kutoka juu kwenda chini tena na kuziachanisha tena kuta za kike na kufunika ua zima kwa kinywa chake. Kwa sekunde chache ulimi wake ulitembea taratibu kuliko nilivyotarajia, ulitembea kama kisu cha daktari bingwa upasuaji, ulitembea kama tabibu bingwa wa moyo. Ulichezea kuta zangu kwanza bila kuweka presha kubwa kwenye lulu ya uanamke wangu. Aliigusa lulu!
Lulu ikagusika
Lulu ikahamasika
Lulu ikaitika
Beee!

Na sauti ikanitoka;

“Aaaah, Freddy, Freddy” nilibakia nalalamika, mikono yangu nimemshika kwenye zake za kirasta ambazo wakati huo zilikuwa zimefunguka na kujiacha upande na upande wa kichwa chake. Alikiinua kichwa chake kuniangalia.
“Nini mpenzi” aliniuliza na kunirushia tabasamu la moto. Kabla sijafanikiwa kusema tena alirudi na safari hii aligusa kuta zangu kwa ulimi wake na kuichukua lulu kama peremende kinywani mwake. Nilijisikia kutetemka. Sijui ataivuta, sijuita atafanya nini. Alijua anachofanya, kwa ulimi wake aliikandamiza kidogo na kuisugua bila kuivuta kwa nguvu, ulimi wake ukaingia kama kwa kuchungulia ndani ya malango ya kasri hilo. Kama umeme mshindo wa mahaba niliusikia ukianza kujijenga tumboni. Nilijiambia kuwa akiendelea kidogo tu atanifanya niachilie volcano ya mapenzi ilipuke. Nilitaka ilipuke akiwa ndani yangu kabisa.

“Basi Freddy, ntakuja sasa hivi” nilimuambia kumbeleza asinifikishe namna hiyo. Aliondoa kichwa chake baada ya kukomba tena kwa ulimi waridi zima! Nilimtia kucha mabegani! Akaja juu yangu huku miguu yangu ikiwa imechanuliwa kama kuku anayebanikwa. Alijiinamisha kunibusu tena.
“Naomba nipe basi Freddy” nilimwomba, alijua ninachotaka, na alikuwa tayari kunipa. Alikuwa kweli tayari kunipa.

“Ntakupa yote” aliniambia. Niliyafumba macho yangu kumsikiliza. Mara akafungua droo ya kitanda na mimi nikafungua macho yangu kumuangalia. Alichukua kuchukua condom ya Trojan XL mikononi mwake. Aliitoa ndani ya paketi yake taratibu na kuhakikisha kucha zake haziiguzi bila kutoboa. Alihakikisha hewa iliyoko kwenye ncha

inazidhibitiwa ili kuhakikisha kuwa condom haiwi na hewa ambayo ingeweza kuipasua wakati wa shughuli. Mkono wake mmoja ukiwa umeshikilia kwenye ncha mkono kwa mkono mwingine akaanza kujivisha kwa kuivingirisha vizuri hadi mwisho kabisa wa mtalimbo wake. Akaachilia ncha ya condom, ilikuwa imekaa sawasawa na vyema kabisa.

Kama mfalme ambaye alikuwa anaingia kwenye hekalu ambalo yeye ndiye mrithi wake pekee wa daima, maungo yake ya kiume yaligusa malango yangu taratibu na kuta zangu zikapisha na kujiachia. Kama kisu kikali kikichoma embe dodo lililowiva na kuacha michuzi ikimwagika kila upande ndivyo ilivyokuwa katika eneo la tukio. Aliingia taratibu na kwa upole, aliniingia kama mtaalamu wa mapenzi, alizama kama sime alani. Sikuhisi mwisho wake wa uume wake ndani yangu, alikuwa bado ananiingia. Nililalamika kwa mapenzi na alipozama kabisa niliifunga miguu yangu nyuma ya kiuno chake kuhakikisha hatoki. Alizungusha mikono yake chini yangu na kuikutanisha mgongoni kwangu. Ya kwangu ilikuwa imefungwa nyuma yake pia. Tulikuwa tumekumbatiana.
Wakati huo huo wimbo wa Bryan Adams “Lets make a night to remember” ulianza kutusindikiza. Pole pole tukaanza kupelekeshana katika vilele vya mahaba. Alianza kunipa mapenzi yake nami nikaanza kumrudishia;

Pigo kwa pigo
Kiuno kwa kiuno
Mguno kwa mguno
Mguso kwa mguso

Mimi na mjamaika wangu. Alianza kuongeza mwendo, nilimechisha, alipopunguza niliongeza, alipojaribu kuvuta kwenda juu nilimvuta chini. Midomo yetu ilikuwa bado inasalimiana na kupeana “hi”. Nilishindwa kuendelea kumbana miguuni, niliamua kuiachia miguu yangu. Freddy alipata nafasi.

Alianza kunipa mapigo ya Kiluguru, mapigo ambayo nilikuwa nayasikiliza hadi kwenye nyusi na kwenye nyayo. Nilishindwa kujizuia.
“Samahani Freddy, kwa nilivyokutenda” nilikuwa nalia
“Bwana yalishaisha yale” aliniambia huku akihema kwa nguvu
“I know baby, lakini unisamehe, nataka nikupende milele” nilifanikiwa kusema.
Freddy hakunihurumia, alizidi kunipa. Nilipokea vyote furaha na kwa fahari. Kwa sababu alikuwa tayari kunifikisha nilijikuta nazidiwa na nikashindwa kujizuia.
“Mpenzi nakaribia kufika” nilimuambia kwa sauti ya kumnong’oneza lakini ya haraka.
“Hata mimi baby” alisema huku akiongeza mwendo, na mimi niliongeza kwa sekunde kama kumi na tano tulizama katika kusikilizia miili yetu ikijibizana, tulikuwa tumeloa chapachapa, tulikuwa tunabusiana na kupeana vituz kwa namna ya kushangaza. Ilikuwa ni patashika.

“Aahh baby nakuja” alilamika
“Njoo mpenzi njoo” nilimuambia kwa kumualika nikampa *signature* yangu ya mauno, signature ambayo siwezi kusimulia maana watu wanaweza kuiigizia bure wakaniibia Freddy wangu. Nilimkatikia kwa namna ambayo ni mume wangu tu amewahi kuishuhudia. Kila mwanamke anayo signature yake

ambayo anajua akiitumia mwanamme anakuwa hoi. Nilipoirudia katika kipeuo cha pili, Freddy alishindwa kuendelea alijiachia full shangwe na mimi nikamkolezea kwa double signature ambayo iko copyrighted! Nikajiachia!!

“Aaahh” nilipiga kelele wakati Freddy naye akiguna tukiwa tumekumbatiana na tukifika kwa pamoja kileleni. Nilimsikia kuhema kwake na alisikia kuhema kwangu, moyo ulikuwa unadunda kwa kasi. Tulikuwa bado tumekumbatiana.

Sayari zote ziliacha kuzunguka wakati ule, wadudu waliao usiku walinyamaza ghafla; sikusikia mlio wa mbwa nje wala wa paka. Kwa heshima upepo uliokuwa unavuma nje ulikoma ghafla. Ni kweli tulikuwa katika kilele cha mahaba. Kati yetu na dunia kulikuwa ni mawingu ya raha. Nieleze vipi ikaeleweka, Wagiriki wa kale wangeweza kuelezea kuwa yalikuwa ni mabusiano kati ya mtoto wa miungu na mwanadamu.

Mikononi mwake lilikuwa ni kumbatio la moyo wangu, lilikuwa ni kumbatio la mapenzi, kumbatio la aliyetambua makosa yake, kwa kweli kabisa katika mlipuko wa mahaba yale tulikuwa tumeshikana na kung'ang'aniana kama mlio wa kinanda ukichezwa vidole; lilikuwa ni kumbatio la mwenye makosa. Hatimaye nilijua kweli nimesamehewa. Lilikuwa pia ni kosa lenye heri kwani lilinipa penzi namna hiyo. Penzi la kifalme na kishujaa. Sekunde hizo mikononi mwake zilikuwa ni kama umilele. *Muungano na udumu!!!*

Aliponiachilia alijichomoa taratibu huku mkono wake ukiwa umejishikilia kuhakikisha condomu haichomoki na hazina yake. Toba yalikuwa ni *mafuriko.* Aliichomoa mwilini mwake na kuelekea moja kwa moja msalani ambako aliitupa. Nilikuwa bado nimelala chali najisikilizia. Alirudi na kulala pembeni yangu. Kwa dakika chache hivi nilikuwa bado mikononi mwake.
“Freddy” nilisema
“Tina” aliniitikia.
Sikuwa na la kusema, nilitaka nimuulize mambo mengine mengi, nilitaka nimjue zaidi. Sikuwa na kauli. Niliishiwa nguvu kabisa nikajikuta nazungusha mikono yangu kwake na kumkumbatia tena. Tukiwa uchi wa nyama tulipitiwa na usingizi huku mioyo yetu ikizungumzishana na kuelewana. Ilikuwa ni sauti kutoka kilindi kwenda kilindi kingine na huko hata kauli hazitoshi.

Saa saba kamili niliamka. Freddy alikuwa bado amelala usingizi. Nilienda bafuni na kujisafisha na kuoga tena. Niliporudi nilianza kuvaa nguo zangu taratibu huku moyo wangu wote ukiwa una hamu tena na tena na Freddy. *Hii haiwezi kuwa mwisho leo.* Nilijiambia. Mahangaiko yangu yalimuamsha Freddy.
“Vipi mpenzi” aliniuliza akipapasa macho yake.
“Baby inabidi nirudi vinginevyo nitapitiliza hapa” nilimuambia kwa moyo wa majonzi. Nilitamani nilale pale ili nimpe mapenzi usiku kucha. *Labda siku nyingine.*
Aliamka na kuanza kujiandaa na yeye baada ya kwenda kujimwagia haraka haraka. Alipomaliza na mimi nilikuwa tayari, akanivuta tena na kunibusu na kuanza kulegea tena.
“Freddy nisipoondoka ntahamia” nilimuambia. Alikubali na kuanza kunisindikiza.
“Umenipa furaha beyond measures” aliniambia.

“Me more darling” nilimwambia. Alifungua mlango wa nyumba yake na kuniongoza kwenye gari lake nilipoingia tu kwenye gari alienda na kuwafungulia mbwa ambao walimsindikiza hadi nilipokuwa kwenye gari. Alifungua geti na kulisogeza gari nje tu hapo na kwa haraka akafunga geti nyuma yake. Alianza kunirudisha Blue Pearl ambako nilikuta gari langu likiwa salama salmini likinisubiri. Tulizungumza mawili matatu lakini kutokana na uharaka sikutaka tuzungumza muda mrefu sana.

Baada ya Freddy kuniacha nikiwasha gari langu aliondoka. Na mimi nilitoka hapo na kuelekea kwenye harusi ya mtoto wa rafiki yetu ambayo bado ilikuwa ndio inanoga kwenye ukumbi wa hapo hapo Ubungo Plaza. Nilihamisha tu gari na kulisogeza upande ukumbi wao wa sherehe. Nilitoka ndani ya gari nikiwa nimeshika zawadi na kuingia ndani. Ilikaribia saa nane za usiku. Nilipoingia ndani nilijionesha onesha na kutoa udhuru kuwa nilikuwa kwenye shughuli nyingine katikati ya jiji kuhusiana na sherehe za Muungano. Hakuna aliyejali sana. Sikukaa sana kwani nilikuwa nataka nifike nyumbani mapema kidogo. Baada ya kama dakika kumi na tano hivi nikaaga baada ya kupiga soga kidogo na maharusi ambao walikuwa wanapumzika kutoka katika kusakata rumba. Walifurahi sana kuniona. Na mimi vile vile nilifurahia kuwaona. *Ndoa.*

Niliondoka na kuingia kwenye gari langu na kuanza kukanyaga mafuta kuelekea nyumbani. Nilikuwa nimechoka mwili lakini akili yangu ilikuwa imechangamka mno. Nilikuwa nacheka na kufurahia na kutoamini nilichofanya siku ile. Kila nikikumbuka muziki, bafuni, kitandani nusura nipige makelele ndani ya gari. Nilipiga kelele ya furaha. Sikuwahi kutarajia kama kuna mtu angeweza kuyagusa maisha yangu namna ile. Nilimshukuru Mungu (msiniulize kwanini) kwa kumleta Freddy ndani ya maisha yangu ambaye alikuwa ni kama malaika wa uvuvio. Aliufungua moyo na mwili wangu uliokuwa umefungwa kwa karibu miezi saba. Alinifanya nijisikie mwanamke tena. Nikiwa naendesha gari kuelekea nyumbani kuelekea nyumbani usiku huo wa manane nilijikuta naimba wimbo mmoja ambao sijauimba kwa miaka; sijui kwanini ulinijia, na sitaki kuhojiwa kwanini niliimba usiku wa giza tena barabarani. Sikuimba wimbo wote isipokuwa kibwagizo chake tu, natamani nikuambie wimbo wenyewe lakini hautanielewa. Haukuwa wa mapenzi – itoshe tu kusema ilikuwa ni pambio.

Nilipofika nyumbani walinzi walinifungulia na kunisalimia. Niliegesha gari na kuingia ndani tena moja kwa moja chumbani juu. Waziri alikuwa bado kwenye sherehe za muungano. Niliingia bafuni na kujimwagia tena maji huku nacheka na kujicheka. Nilipomaliza nilijirusha kitandani kulala. *Usiku wa kukumbukwa.* Usingizi ulianza kunichukua taratibu na nilipitiwa ndani ya nusu saa. Kabla ya kupitiliza nilishtuka. Sikuw nimemtumua ujumbe Freddy kuwa nimefika salama nyumbani anaweza kuwa alikuwa na wasiwasi. Nilichukua simu yangu na kumtumia ujumbe kuwa nimefika salama kabisa na kumwandikia hisia zangu kutoka moyoni. Niliamua kumuandikia kwa Kiingereza.

Dear Freddy, you are really awesomely passionate, you leave me speechless, you turn tears into happy bliss, you make bad things seem not so bad. You astonish me and you brighten every aspect of my life. Like you said, it’s amazing that we’ve grown so close in such a short amount of time. The feelings

blossomed rapidly and I don't want to lose that. I have fallen madly in love with you. You would make me happier than the richest person in the world by sharing your love with me.

I know I am not perfect, but I do have goals in my life. I take good care of myself and my work. I am honest, sincere, and true, and I have a lot of love to give if you are willing to be on the receiving end. Please take this to heart, Baby; I love you.

I don't know this feeling - I have never experienced it. I want you by my side. I could never get tired of being near you.

For always, for love

C'Tina!

Sikusubiri majibu. Nililala kama mtoto mchanga.

* * *

“Mama Renatus” mume wangu aliniambisha kwenye saa tatu hivi za asubuhi. Sikumbuki aliingia nyumbani saa ngapi.
“Bee!” Nilimuitikia kiuvivu.
“Huendi kanisani leo” aliniuliza akiwa amejilaza bado kitandani pembeni yangu.
“Sidhani *mpenzi,* mwili umechoka kweli” nilimuambia. Kwanini nilimuita mpenzi. Sijui.
Alishtuka kidogo kwa kuguna. Alinigeukia na kunibandika busu shavuni. Aliondoka kuelekea bafuni na kujiandaa kwenda kanisani. Nilibakia kuuchapa usingizi kwa karibu masaa mawili mengine. Nilipoamka ilikuwa saa tano za asubuhi, mume wangu bado alikuwa hajarudi kutoka kanisani pale Usharika wa Kiluvya.
Nilipomaliza kuoga na kutulia kitu kimoja kilianza kunisumbua mawazoni. Nilikosa amani kabisa na kujisikia mpweke kabisa. Nilitamani kupiga kelele ya kilio. Nimefanya nini mimi. Ni kama wingu zito liliondolewa kichwani mwangu na kama pazia la giza liliinuliwa. Mara moja kitu kilichokuwa nyuma ya fikra zangu kilikuja kwenye akili zangu kwa mwanga mkali kama gari linapomulika machoni usiku. *Kuna kitu si sahihi kuhusu Freddy!*

Sikujua ni kitu gani, sikuweza kukipatia mara moja lakini kengele zote za tahadhari kichwani mwangu zilianza kupiga kelele kwa nguvu. Freddy ni nani? Anataka nini kwangu? Kwanini kuna vitu ambavyo sivielewi kwake. Mbona anapoishi ni tofauti kabisa na shughuli anazofanya. Ameweza vipi kufika alivyofika kwa kuuza tu kwenye kibanda. Wazazi wake ni nani? Basi mtiririko wa mawazo ulianza kunijia kwa nguvu na maswali lukuki yaliyopangiana utadhani nimeitwa Polisi. Nilijisikia kutetemeka. Nimeisaliti ndoa yangu; nimefanya kile ambacho sikutarajia kufanya maisha yangu yote. Mume wangu akija kujua itakuwaje, nitaharibu kazi yake, na watoto je. Machozi yakaanza kunilenga. Nilijisikia vibaya kupita kiasi.

Niliamua wakati huo huo kuwa kwani Freddy alikuwa anajua nini cha kweli kuhusu mimi. Kama kuna kitu alikuwa anaficha kuhusu yeye na mimi kulikuwa na vitu ninavificha. Zaidi ya jina langu hakuwa anajua mengi kuhusu mimi, mume wangu au familia yangu. Nilifurahia mapenzi aliyonipa jana lakini nilijua nisingeweza kuendelea naye tena. Sikuwa tayari kuendelea naye. Kama ni msamaha nilikuwa nimemuomba na

akanipa kwa namna ya kukumbuka. Nisingeweza kumuona tena mjamaika wangu. Nilidhamiria.

Nikiwa na mawazo hayo nilisikia ngurumo ya gari la mume wangu likiingia ndani ya eneo letu. Mume wangu. Nilijisikia kumpenda kuliko wakati mwingine wowote. Nilitamani aingie ndani nimkumbatie na kumuomba msamaha kwa kumnyima kile nilichojipatia miye jana. Nilitamani nimuombe msamaha na yeye kwa namna ya kumzidi Freddy. Alikuwa anasalimiana na walinzi pale nje na kuangalia mambo mawili matatu. Alifika mlangoni ambako alinikuta namngojea.

“Mpenzi karibu” nilimuita tena mpenzi, alisita kidogo. Alinipa busu mdomoni nililikubali. Hakuamini.
“Mbona umechangamka” aliniuliza. Nilitamani kumueleza kwa undani, nisingeweza.
“Hamna neno dear” Nilimrudishia busu. Nilikuwa nimemsamehe kwa namna ambayo sikutarajia na kwa njia ambayo haikuwa katika mpango wangu. Freddy alikuwa hajanibu sms yangu ya jana. Nilishukuru. Baba Renata aliingia na kwenda ghorofani kubadili nguo na kuwa katika mavazi ya kutulia tu siku ya Jumapili. Alipanda ngazi huku anapiga mluzi wa *neema, neema, neema imefunuliwa!*

Lazima nivunje uhusiano na mjamaika. Wakati wazo hilo linanipitia simu yangu iliyokuwa mezani ilitetemeka kuashiria kuna sms imeingia. Niliichapukia kabla haijaita tena. Nilibonyeza kusoma ujumbe wake.

“Hi baby, thanks for the message, I'm absolutely and deeply into you! I feel the same way and more than I could explain it. I have to tell you and show you”. Aliniandikia. Nilijikuta nauliza “ya kweli hayo?” nilisahau kwa sekunde mpango wa kum*delete* kwa jumla ili niokoe ndoa yangu.
“Absolutely, unafanya nini Mei Mosi?” ndio ulikuwa ujumbe wake. Mei Mosi ilikuwa ni Jumamosi iliyofuata. Ameniuliza *nafanya nini Mei Mosi*? Well.. pigo juu ya pigo, kiuno juu ya kiuno, mguso juu ya mguso na busu juu ya busu! Ameniuliza nafanya nini *Mei Mosi?*

Nilijua nitafanya nini.

Mume wangu alikuwa anamalizia kushuka ngazi. Nilitabasamu tulipogonganisha macho yetu.

MWISHO

KANUSHO:

Hadithi hii ni simulizi la kutunga na halina uhusiano na mtu, watu, matukio au mambo halisi yaliyowahi kutokea au yanayotokea sasa. Mfanano wowote na watu, mahali, majina na matukio halisi ni matokeo ya kinasibu tu na si kusudio la mtunzi. Haki zote za kuichapa au kuitoa kwa namna yoyote ile na kwa mtindo wowote ule au kuiwakilisha kama kazi ya sanaa, filamu, vitabu n.k bila idhini ya mtunzi zinashikiliwa na Jamii Media Ltd.



Kama unafikiri umewahi kusoma hadithi za kusisimua basi hujakutana na "Kamanda"!

KUTOKA 'USO KWA USO NA KAMANDA

…

Kama ilivyo sehemu nyingi za ofisi zetu mara baada ya bosi kuondoka watu hushusha pumzi na mara ofisi inageuka na kuwa mahali ambapo paka ameondoka na panya wanapanga viti vyao vya enzi. Beka akaona ni wakati muafaka kwenda kwa mama Mayungi kuzungumza naye kama alivyomwomba awali. Alijihisi hofu kidogo na moyo ulikuwa ukimdunda huku kijasho chembamba kikiteremka makwapani mwake. Alijiambia moyoni kuwa "liwalo na liwe".

"Haya shoga vipi tena?" mama Mayungi alimlaki Beka kwa swali.

"Mama kwanza samahani kama nitakukwaza au utanielewa vibaya" alianza Beka kwa upole huku akiwa amevuta kiti cha mgeni na kusogea karibu na meza ya mama Mayungi, Katibu Mahsusi wa Kamanda Mwaipopo.

Mama Mayungi alikuwa amevalia sketi ya rangi nyekundu ya damu ya mzee iliyompita kidogo tu magotini na blauzi nyeupe ya mikono mifupi iliyochorwa maua madogomadogo ya rangi nyekundu ya damu ya mzee vile vile. Alikuwa amezivuta nywele zake nyuma na kuzifunga vizuri kwa kibanio huku chache zinazoanzia mbele zikionesha kuanza kwa mvi ikiwa ni ishara ya umri wake ulioenda. Hereni kubwa za mviringo za rangi ya dhahabu zilikuwa zikining'inia katika masikio yake.

Hakuwa mzee kwa kipimo chochote kile; alikuwa ni mama wa makamo. Utukufu wa ujana wake ulikuwa bado unang'ara katika sura yake.

"Utanikwaza kwa lipi Beka, haya niambie nini kimekusibu maana umeniweka roho juu kutwa nzima" mama Mayungi alisema huku akiacha kuchapa kwenye kompyuta kazi aliyokuwa nayo. Upande wa mlangoni watumishi wengine waliendelea kuchomoka mmoja mmoja toka katika ofisi zao huku mlio wa kengele ya lifti ukisikika kwa mbali ikichukua wafanyakazi kuwapeleka chini.

"Sijui nianzie wapi; lakini naomba usinielewe vibaya" Beka alianza na kusita kwa sekunde chache. Mama Mayungi alimuangalia kwa udadisi bila kusema lolote.

"Nina mtihani mama Mayungi; mtihani ambao sijui utaishia vipi maana ni mkubwa." Alisema na kukatisha akiyaacha manenyo yake hayo yazame katika fikra za mama Mayungi. Aliendelea "Kamanda Mwaipopo amenitaka kimapenzi" alisema hilo kama mtu aliyetua mzigo mzito uliokuwa ukimuelemea. Alijua kuwa tayari maji ameshayamwaga hapo.

"Mungu wangu! Beka *are you serious*"? mama Mayungi aling'aka na kuuliza kwa wakati mmoja.

"Sitanii mama Mayungi na kwa kweli inaniweka katika hali tata kwa kweli" alijibu Beka huku akishusha pumzi na kukutanisha viganja vya mikono yake, vidole vyake vilikumbatiana.

"Na wewe unamtaka?" mama Mayungi alihoji huku sauti yake ikiwa kavu. Alianza kukusanya makaratasi mbalimbali yaliyokuwa mezani huku akisubiri jibu la Beka.

"Hapana mama Mayungi, si unajua nina mume wangu na ni mwaka mmoja tu wa ndoa tumeanza?; siwezi wala sijafikiria kitu cha namna hiyo" Beka alijibu kwa maneno yenye uhakika na kujiamini. Sauti yake ilikuwa thabiti, ya upole lakini iliyoficha wasiwasi na woga.

"Umemjibu nini?" mama Mayungi aliuliza.

…

* * *

Hadithi hii mpya ya "Uso kwa Uso na Kamanda" itakujia baada ya wiki chache zijazo. Itapatikana tu kwa mchango kidogo kwa kufidia muda na vipaji. Pamoja na kisa kingine kingine cha kusisimua (bonus) vyote vikipatikana kwa barua pepe TU kama tulivyofanya kwenye ripoti ile ya Meremeta.

Itaweza kupatikana kwa mchango kidogo kwenda JamiiForums ambapo kiasi kitabakia kusaidia JF kwa kukubali kuwa njia ya kuweza kukusanya malipo haya. Utaweza kulipia kwa njia ya simu – vocha na kwa walio nje ya nchi wataweza kujipatia kisa hiki kwa njia ya paypal na kadi za kibenki (fuata maelekezo chini)

Ili uwe wa kwanza kujulishwa kuwa kisa hiki kipya kiko tayari na kuweza kujipatia nakala yako jiunge nami kwenye Facebook - "Mzee Mwanakijiji" au niandikie mwanakijiji@jamiiforums.com kutaka uwe miongoni mwa

watakaojulishwa utaratibu wa kukipata kisa hiki kipya na kinachokwenda na wakati.

Kwa sasa ni mchango wa 7.99USD or 5.50£ au 8,000Tsh kwa mtu mmoja. Tafadhali si kwa ajili ya kusambaza kwa wasiolipia. Waunge mkono wasanii wenu.
Anza kujitolea kwa kutuma credit za simu za kiasi hicho kwenda namba 713-444-649 na utume email ya kunijulisha pia kwenda Mwanakijiji@jamiiforums.com ili kutusaidia kuoanisha mahesabu na upate jibu kutoka kwangu pia kuwa zimefika. Hadithi hii mpya itakuwa tayari ndani ya wiki mbili (katikati ya June) kwa waliochangia tu namna hiyo.

MMM - Mtunzi

1. Kwa walio nje wanaweza kutumia PayPal au Credit Cards au Debit Cards kwa kufuata link hii (**http://www.jamiiforums.com/payments.php**) iliyo kwenye sahihi yangu (linapoonyesha dole gumba) na pindi mchangiaji anapoweka chochote tunakuwa notified nasi tunafanya kuwasiliana na mhusika ili aweze kupandishwa kwenda katika group la Premium Members.

Paypal users:

Send via email - **macdemelo@gmail.com** moja kwa moja itafika na utaarifiwa ndani ya dakika 60 kuwa mchango wako umepokelewa.

2. Njia ya pili ni kutumia Western Union au Money Gram na kutuma kwenda kwa Maxence Melo Mubyazi wa Dar es Salaam.

3. Njia ya tatu ni kutumia Bank accounts za Maxence kama ifuatavyo:

NBC:

Acc #: 033201064359
Jina: Maxence Melo Mubyazi

CRDB:

Account Name: Maxence Melo Mubyazi
Bank: CRDB Pugu Road Branch
Swift Code: CORUTZTZ
Acc No: 01J2092391800

4. Njia ya nne:

Unaweza kutuma recharge vouchers za tiGO, Zain, VodaCom au Zantel kwenda kwa Maxence - 0713444649 naye atakufahamisha kuwa kazipokea.

==========

Ikumbukwe, SI LAZIMA kuandika jina lako la kweli na SI LAZIMA kwenda mwenyewe bank kutuma pesa hizo (kwani unaweza kumpa unayemwamini na kumpa account details na jina lako ambalo ungependa aandike).

Tunaweza kuandika mengi lakini ukweli unabakia pale kuwa JF inahitaji michango yenu kwa sana tu.

Kwa wenye maswali zaidi wanaweza kuwasiliana na Maxence kupitia namba yake ya simu: 1 713-444-649